**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA IBADA YA KUMWEKA WAKFU NA KUMTAWAZA ASKOFU WA NNE WA DAYOSISI YA *WESTERN* TANGANYIKA, KANISA LA ANGLIKANA TANZANIA, KANISA KUU LA ANDREA MTAKATIFU, KASULU KIGOMA, TAREHE 30 JANUARI 2022**

- Mhashamu Baba Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania Dkt. Maimbo William Fabian Mndolwa;
- Mheshimiwa Lay Canon Wakili George Mandepo, Msajili wa Kanisa Anglikana Tanzania;
- Wahashamu Maaskofu wote wa Dayosisi za Kanisa Anglikana Tanzania mliopo hapa bila kuwasahau Wahashamu Maaskofu Wastaafu;
- Wahashamu Maaskofu kutoka nchi jirani ya Jamhuri ya Burundi;
- Mhashamu Baba Askofu Emmanuel Charles Bwatta, Askofu wa Nne wa Dayosisi ya Western Tanganyika uliyewekwa Wakfu muda mfupi uliopita;
- Viongozi wa Madhehebu mengine ya Dini mliopo hapa leo ikiwa ni pamoja na Mhashamu Askofu Joseph Mlola, Katibu Mkuu wa AICT;
- Katibu Mkuu wa CCT, Mchungaji Canon Dkt. Mosses Matonya;
- Mheshimiwa Kamishna wa Polisi Thobias Andengenye, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma;
- Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Makamba, Jamhuri ya Burundi;
- Viongozi wote wa Serikali;
- Waheshimwa Wabunge wote wa Kigoma, wakiongozwa na Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Mbunge wa hapa Kasulu Mjini;
- Viongozi wa CCM na Vyama Vingine vya Siasa;
- Mama Jusiline, Mke wa Mhashamu Baba Askofu Emmanuel Bwatta;
- Familia na ndugu wote wa Mhashamu Baba Askofu wetu mpya;
- Wachungaji, Mashemasi na Waumini wote wa Kanisa Anglikana;
- Waheshimiwa Wageni Waalikwa wote kutoka ndani na nje ya Tanzania;
- Mabibi na Mabwana.

**BWANA YESU ASIFIWE!**

Awali ya yote na kwa unyenyekevu kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa fadhili na rehema, kwa kutupatia kibali cha kushiriki Ibada hii ya furaha ya kuwekwa wakfu na kutawazwa kwa Mchungaji Emmanuel Bwatta, kuwa Askofu wa Nne wa Dayosisi ya *Western* Tanganyika.

Aidha, kwa nafasi hii pia naleta kwako Mhashamu Baba Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dkt. Maimbo W. F. Mndolwa na Kanisa zima, salamu kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Mheshimiwa Rais alitamani kuhudhuria Ibada hii yeye mwenyewe, lakini kutokana na majukumu mengine ya kitaifa amenituma kumwakilisha.

***Mhashamu Baba Askofu Emmanuel Charles Bwatta,***

Mheshimiwa Rais anakupongeza sana kwa kuwekwa kwako wakfu na kutawazwa kuwa Askofu wa Nne wa Dayosisi hii ya *Western* Tanganyika. Nami naungana na Mheshimiwa Rais na Kanisa zima kukupongeza, kwa kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu kuwatumikia watu wake. Aidha, tunakupongeza pia kwani tunaamini haikuwa rahisi kufikia hatua hii, lakini kwa neema yake Mungu imewezekana. Katika Waraka wa Kwanza wa Paulo kwa Timotheo ***(1 Timotheo 3:1)*** tunasoma ***"Ni neno la kuaminiwa; Mtu akitaka kazi ya Askofu, atamani kazi njema****.* Hivyo, umechagua fungu jema la kuwatumikia watu wa Mungu na tunaamini Mungu ataendelea kuwa pamoja nawe na kukuwezesha katika utume wako. Kipekee ninakupongeza sana Mama Jusiline Bwatta kwa kumpenda, kumuombea na kumsaidia mwenza wako hadi kuitikia wito huu mtakatifu. Sasa yakupasa uongeze mapenzi na sala kwa ajili ya mumeo na familia yako maana bila nyumba imara, utume wake utajaa makwazo na ukumbuke ipo siku utatakiwa kupeleka hesabu mbele ya Mungu.

Aidha, ninawapongeza sana Waumini wa Dayosisi hii ya *Western* Tanganyika kwa kupata Mchungaji Mkuu mwingine, tena kijana mwenye nguvu na ari ya kuwatumika na kuwaongoza kiroho na katika shughuli nyingine za maendeleo ya Dayosisi. Ni imani yangu kuwa mtampatia ushirikiano wa dhati ikiwa ni pamoja na kumtii anapotuelekeza kweli ya neno la Mungu, kumtia moyo na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kumtumikia vema katika kuiletea Dayosisi yenu maendeleo ya kiroho na kimwili.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu,***
***Maaskofu na Wachungaji Mliopo,***

Kazi ya kumwongoza mwanadamu ili afikie kusudio lake Mungu, ni kazi yenye mapito magumu, majaribu na hata taabu. Nina hakika Wahashamu Maaskofu

wastaafu wanaweza kushuhudia haya. Mtume Paulo katika Waraka wa pili kwa Wakorintho (***2 Wakorintho 11:23 - 28***) aliyapitia na alitoa ushuhuda juu ya maisha ya Wahudumu wa Kristo, kwamba ni zaidi katika taabu, vifungo, mapigo, hatari na masumbufu ya kukesha na kufunga mara nyingi.

Rai yangu kwenu Wahashamu Maaskofu, Wachungaji na Viongozi wote wa dini ni kuwa mwendelee kuifanya kazi ya Mungu kwa uaminifu, uhodari na kwa moyo thabiti. Msikatishwe tamaa na majaribu na taabu mnazopitia katika utume wenu. Msitake kujilimbikizia mali isivyo halali au kugombana kwa sababu ya kutaka madaraka zaidi. Kumbukeni Waraka wa Kwanza wa Mtume Petro ***(1 Petro 5:2-3)*** alivyowaasa viongozi wa Kanisa kuwa ***"lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu na kulisimamia, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi".*** Hivyo naomba kuwatia moyo mfanye kazi hii kwa bidii, unyenyekevu na uaminifu mkubwa mkijua ya kuwa ***Mchungaji Mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka*** (**1 Petro 5:4**).

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu,***
***Maaskofu, Waumini na Wageni Waalikwa,***

Naomba hapa niwakumbushe waumini wenzangu kwamba nasi pia tunao wajibu kwa Viongozi wa Kanisa! Tunasoma katika waraka wa Mtume Paulo kwa ***Waebrania 13:17*** kwamba: ***"Watiini wenye kuwaongoza na kuwanyenyekea maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua, maana isingewafaa ninyi".*** Hivyo, rai yangu kwa waumini wenzangu ni kuwa tusiwakwaze Wachungaji na Maaskofu wetu. Tusiwe chanzo au sehemu ya kukuza migogoro katika makanisa na kukwamisha kazi njema ya kutangaza Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu, Maaskofu,***
***Wachungaji, Waumini na Wageni Waalikwa,***

Kwa miaka mingi, Kanisa la Anglikana Tanzania limekuwa na mchango mkubwa sana katika ustawi wa Taifa letu kiroho, kiuchumi na kijamii na limewezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa katika nyanja zote kufikia kuwa nchi ya hadhi ya kipato cha kati (LMIC). Kwa namna ya pekee, Kanisa limekuwa mshirika mkubwa sana wa Serikali katika utoaji wa huduma za kijamii. Kanisa limeshiriki katika kutoa misaada mbalimbali kwa jamii na kushiriki katika shughuli za kiuchumi/kimaendeleo ikiwemo miradi ya vikundi vya vijana na akina mama, kilimo bora na ufugaji wa kisasa

pamoja na biashara. Katika maeneo ya utoaji wa huduma za kijamii, kanisa limeweza kupeleka huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali nchini ambayo Serikali bado haijapeleka huduma hizo hususan vijijini na maeneo ambayo yanahusisha watu wa hali ya chini mijini. Hivyo, Kanisa limewezesha wananchi kupata huduma nzuri za afya na elimu hasa kwa watu wa kawaida, yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu,***

Kama alivyosema Rais kwenye Kongamano la Wachungaji na Maaskofu katika maadhimisho ya miaka 50 ya Jimbo la Kanisa Anglikana Tanzania mwaka jana, amenituma niwaeleze tena kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita anayoiongoza, inatambua na kuthamini sana mchango mkubwa wa Kanisa Anglikana Tanzania, katika kuwahudumia watanzania kiroho na kimwili. Nami naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali kuwapongeza na kushukuru sana Kanisa Anglikana Tanzania na Dayosisi zake zote kwa kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuwahudumia watanzania tena bila ubaguzi. Napenda niwahakikishie kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na Taasisi zote za dini nchini, ili kuziwezesha Taasisi hizo kuendelea kuwahudumia wananchi kiroho na kimwili kwa ufanisi.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu,***
***Viongozi wote na Waumini mliopo,***

Pamoja na shukrani zangu juu ya mambo hayo mazuri yanayofanywa na Kanisa Anglikana Tanzania, kuna maeneo machache ambayo napenda niwaombe, kwa niaba ya Serikali, myapatie msisitizo zaidi katika mafundisho na maonyo yenu. Jambo la **kwanza** ni kulinda na kudumisha Amani, Umoja na Uhuru wa nchi yetu. Tunu hizi za Taifa ndizo zinazotutambulisha sisi kama watanzania popote duniani. Kwa namna ya kipekee kabisa na kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru kwa maombi yenu kwa ajili ya Amani, umoja na ustawi wa Taifa letu. Naamini kuwa ni kutokana na Maombi hayo Mwenyezi Mungu amelifanya Taifa letu kuendelea kuwa kisiwa cha amani na utulivu na kuvuka mapito makubwa bila kutetereka. Hivyo, nawaomba sana viongozi wote wa dini muendelee bila kuchoka kuliombea Taifa letu kuwa na amani na kukemea vitendo vyovyote vinavyoashiria machafuko nchini. Kama mnavyofahamu, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ambayo itakapokamilika itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa. Miradi inayoendelea kujengwa katika mkoa wetu wa Kigoma ni pamoja na barabara (Kazilambwa - Chagu km 36, Uvinza - Malagarasi km 51.1; Kabingo - Kibondo - Kasulu - Manyovu km 260, Kibondo Townlink km 25; kuunganisha mkoa kwenye gridi ya Taifa ya umeme (Mkandarasi tayari amepatikana) na kusambaza umeme

vijijini chini ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA); ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi (VETA); shule na madarasa; hospitali, vituo vya afya na zahanati; miradi ya maji; kilimo cha michikichi; kuboresha masoko n.k. Kufanikiwa kwa miradi hiyo yote inategemea sana uwepo wa amani na utulivu katika mkoa na nchi yetu kwa ujumla. Aidha, amani, umoja na upendo katika nchi ndiyo chanzo cha Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu***,

Jambo la **Pili,** katika miezi na siku za karibuni, tumesikia mfululizo wa matukio katika mikoa mbalimbali ya nchi yetu yanayoonesha kuwa hofu ya Mungu inatoweka ikiwa ni pamoja na mauaji ya kutisha sana!. Katika Jiji la Mwanza, wanawake watatu (mama, mtoto na dada wa kazi) waliuawa kikatili kwa kubakwa, kukatwa mapanga na miili yao kutupwa mtoni uchi!; Wiki iliyopita watu watano wa familia moja nao waliuawa kikatili ndani ya nyumba yao kijiji cha Zanka, Dodoma. Mbeya nako baba mmoja alichinjwa na mwanaye askari! Moshi pia mama mfanyabiashara wa madini alichinjwa na kuuawa na mwili wake kutupwa kwenye shimo la choo! na kadhalika na kadhalika!. Cha ajabu tunasema eti ***haya yote tunamuachia Mungu***! Kweli tunamuachia Mungu ukatili huu uliopitiliza? Kama hayo hayatoshi bado ushoga na ukatili wa kingono upo! Wachawi na Waganga wa Kienyeji wapo kiasi cha kudiriki kumfanya kijana kuwa msukule kama ilivyotokea kule Magu! Biashara ya bangi na madawa ya kulevya bado ipo! Pia uzembe kazini na ufisadi katika Ofisi za Umma yote yapo na baadhi ya wahusika ni Wakristo! Pamoja na jitihada za Serikali za kupambana na maovu haya, naliomba sana Kanisa likemee kwa nguvu zote uovu huu na kuongoza waumini kufanya toba ya kweli maana matendo hayo ni chukizo kubwa kwa Mwenyezi Mungu. Fundisheni kwa nguvu na mamlaka, maadili mema kwa vijana wetu dhidi ya tamaa ya kujipatia mali haraka kwa njia zisizo halali.

***Mheshimiwa Baba Askofu Mkuu***,

Jambo la **Tatu** ambalo naomba mlitilie mkazo ni usafi na utunzaji wa mazingira. Tunaomba Viongozi, Kanisa na madhehebu mengine yote ya dini kupaza sauti kuhamasisha ulinzi na uhifadhi wa mazingira katika nchi yetu. Ni vema kukemea ukataji na uchomaji hovyo wa misitu na uchafuzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali. Tuwahimize wananchi wote na hususan jamii za wafugaji kuheshimu mazao ya wakulima na kutunza vyanzo vya maji. Tukumbuke katika kitabu cha mwanzo (**Mwanzo 2:15**) tunasoma kuwa, ***"Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza***". Hivyo, nawaomba ninyi mlio mawakala wa Mwenyezi Mungu hapa duniani muwaongoze waumini na kuwahimiza kuitunza na kuilinda ekolojia ya nchi yetu nzuri kwa kutunza

misitu na kupanda miti rafiki na maji, miti ya biashara kama mbao, matunda na miti dawa; na kufanya usafi wa mazingira yetu wakati wote.

***Mhashamu Baba Askofu Emmanuel Bwatta,***

Jambo la **Nne,** Serikali inatambua kuwa maendeleo ya Kanisa hayawezi kuja bila kuwepo na ushirikiano baina ya Kanisa na madhehebu mengine ya dini na pia Serikali. Nikuombe Mhashamu Baba Askofu Bwatta katika kipindi chako cha Uaskofu wa Dayosisi ya *Western* Tanganyika uimarishe zaidi ushirikiano na viongozi wa madhehebu mengine ya dini hapa Mkoani Kigoma na uendelee kushirikiana pia na Viongozi wa Serikali. Napenda nikuhakikishie kuwa, Serikali katika ngazi ya Taifa/Mkoa/Wilaya, tutakupatia ushirikiano unaohitajika katika kutekeleza majukumu yako kwa Mungu, waumini na watanzania kwa ujumla. Ni Imani yangu kuwa, Viongozi wa madhehebu mengine ya dini, Viongozi wa Vyama vya Siasa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali watakupatia ushirikiano wa dhati. Aidha, nawaomba Maaskofu na Wachungaji wengine mliopo hapa leo, kwenda kuimarisha ushirikiano na madhehebu mengine ya dini na Serikali katika maeneo yenu ya utumishi.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu, Maaskofu, Wachungaji, Waumini na Wageni Waalikwa,***

Jambo la **Tano** ni kuhusu migogoro ndani ya Makanisa na Madhehebu mbalimbali ya dini. Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na wimbi la migogoro ndani ya taasisi na madhehebu ya dini mbalimbali inayochafua taswira ya ukristo/dini husika. Nilipokuwa naandaa hotuba hii kuna sehemu nilisoma kichwa cha habari kisemacho "***Bundi anaendelea kuliandama Kanisa***"! kila kukicha nasoma kwenye vyombo vya habari na mitandao kuwa, Dayosisi fulani wamkataa Askofu/Mchungaji au waumini wampiga Askofu tena kwa fimbo yake ya Kiaskofu! Kama hiyo haitoshi, wanamzomea na kumkimbiza! Mnafahamu Dayosisi ya Viktoria - Nyanza ilikaa miaka minne bila Askofu. Aidha, Dayosisi ya Dar es Salaam imepoa baada ya Mhashamu Baba Askofu Jackson Sostenes kusimikwa na kuwekwa Wakfu. Hata hivyo, kwa taarifa tulizonazo Serikalini, moshi unafukuta katika Dayosisi chache ambazo mnazifahamu na siyo lazima kuzitaja hapa. Baba Askofu Mkuu na Maaskofu wote, ninawasihi mkazime fukuto hilo kabla moto haujalipuka. Migogoro hii inalitesa sana Kanisa. Mimi nikifuatilia, huyu bundi ana sura nne: **(i)** Ni matumizi mabaya ya fedha, mapato na mali za Kanisa; **(ii)** Matumizi ya madaraka kinyume na katiba ya Kanisa; **(iii)** Kuminywa kwa haki na stahili za Wachungaji na mafao ya Viongozi wastaafu; na **(iv)** Uchu wa madaraka, ubinafsi na kuendelezwa kwa makundi baada ya uchaguzi katika Kanisa. Yatupasa tutafute dawa ya kuua bundi huyu. Mambo haya yanayolivua nguo Kanisa.

Nitumie fursa hii kuwasihi viongozi wa dini kushughulikia migogoro inayojitokeza kwa kuzingatia sheria za Kanisa na miongozo ya imani ya kikristo au dini yeyote husika na taratibu zinazokubalika. Serikali kwa upande wake itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi na madhehebu yote ya dini nchini ili kuhakikisha yanafanya kazi kwa amani na utulivu na kwa mujibu wa sheria.

***Mhashamu Baba Askofu Emmanuel Bwatta*****,**

Nimefuatilia na nimeambiwa kuwa, wewe umekuwa mchungaji mwadilifu na ulichaguliwa kuwa Askofu kwa haki na si kwa rushwa. Niwie radhi, najua sina mamlaka hata kidogo ya kukupangia kazi lakini, kwa heshima, naomba niseme waziwazi dosari moja ninayoiona hapa kwetu. Jengo hili la Kanisa Kuu limechakaa tena linavuja! Sijui Mt. Andrea msimamizi wa Kanisa hili angetokea hapa leo tutakuwa na maelezo gani kwake! Nakuomba katika kazi zako za mwanzo, kama itakupendeza, iwe ni pamoja na kuhamasisha watu wa Mungu wa Dayosisi ya *Western* Tanganyika kujitoa kwa hali na mali kufanya ukarabati mkubwa wa Kanisa Kuu. Na kwa heshima aliyonipa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumwakilisha katika Ibada hii takatifu nachangia kianzio cha **Shilingi milioni tano**.

***Mhashamu Baba Askofu Mkuu, Maaskofu,***
***Wachungaji na Wote mliopo hapa,***

Naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kusema kwamba, kwa niaba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba yangu binafsi nakutakia wewe Mhashamu Baba Askofu Emmanuel Bwatta, huduma njema na utumishi wako ukawe imara. Uongozi wako ukawe uongozi unaoacha alama chanya ya kiroho na kijamii katika maisha ya kila siku ya waumini na wananchi wa Dayosisi ya *Western* Tanganyika na Tanzania kwa ujumla. Ukawe kiongozi unayewaunganisha waumini na kuwaongoza kuwa watu wema na waadilifu. Mungu akujalie na kukuwezesha kuwa Askofu mtumishi na anayekiri kwa mafundisho na mwenendo, kuwa Yesu Kristo pekee ndiyo mkuu na muhimu zaidi katika huduma na maisha yako na kwamba Kanisa ni kubwa kuliko wewe binafsi. Yeye aliyekuumba tumboni mwa mama yako aujalie Uaskofu wako uwe Baraka na neema kwa Dayosisi ya *Western* Tanganyika na kwa Kanisa lote la Mungu.

**BWANA YESU ASIFIWE!**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**